

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Mtaa wa Bagara Miomboni,
S.L.P. 386,
27103 MANYARA,
Barua Pepe: rbcmanyara@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

MANYARA – JANUARI 15, 2021

**MWENYEKITI BODI YA WAKURUGENZI RIVACU LTD
APANDISHWA KIZIMBANI**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoani Manyara imemfikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Manyara aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Chama Cha Ushirika cha Rift Valley Cooperative Union Limited (RIVACU LTD) Lohay Langay.

Lohay amefikishwa Mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Wakili Martini Makani na kufunguliwa kesi ya Uhujumu Uchumi Namba **1** ya Mwaka **2021** ambayo ipo mbele ya hakimu Mheshimiwa Jumaa lakini kwa leo imesomwa na hakimu Mheshimiwa Kimario kwa sababu Mheshimiwa Jumaa hakuwepo Mahakamani.

Wakili Makani aliiambia Mahakama hiyo kwamba, mnamo tarehe 1 Novemba, 2017 katika ofisi za Chama Kikuu Cha Ushirika cha RIVACU, Wilayani Babati Mkoani Manyara, mshitakiwa akiwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi RIVACU LTD kwa makusudi mshtakiwa alitumia nafasi yake vibaya kwa kuingia mkataba wa ajira na Paulo Makoye.

Katika mkataba huo Makoye aliajiriwa kama Mhasibu wa Chama Kikuu Cha Ushirika (RIVACU LTD) bila kibali cha Bodi ya Wakurugenzi na kujipatia bila kustahili jumla ya shilingi milioni sita na laki mbili (Sh.6, 200,000/=) kitendo ambacho ni kosa chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya 2007. Mshitakiwa alikana mashtaka yake yote na yuko nje kwa dhamana ya shilingi milioni saba (Sh. 7,000,000/=) hadi tarehe 10/02/2021 kesi hiyo itakapotajwa tena mahakamani hapo.

Ni Rai yetu kwa viongozi wawe wa kuchaguliwa au kuteuliwa katika utekelezaji wa majukumu yao watekeleze kwa uadilifu na uaminifu kwa kuzingatia mipaka iliyoainishwa na Sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza maeneo waliyokasimiwa. Kutokufanya hivyo inaweza kupelekea kuchukuliwa hatua za kisheria kama ilivyotokea kwa Lohay Longay kwa kuwa sheria ni msumeno hukata mbele na nyuma.

Imetolewa na:

**HOLLE MAKUNGU
MKUU WA TAKUKURU (M)
MANYARA**